

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 58 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** DESEMBA 2025

NAIBU WAZIRI KWAGILWA AAGIZA TSC KUHAJIKISHA UWIANO SAWA WA WALIMU NCHINI



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Reuben Kwagilwa (kushoto) akisalimiana na Mwenyekiti wa Tume, Prof. Masoud Hadi Muruke katika ziara yeye ya kukutana wa Wajumbe na watumishi wa Tume tarehe 25 Novemba 2025.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

 Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

 [tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

TSC IENDELEE KUTILIA MKAZO JUKUMU LA KUFANYA TAFITI KUHUSU WALIMU

Tunampongeza Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mhe. Reuben Kwagilwa, kwa kuweka msisitizo mkubwa juu ya umuhimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kufanya utafiti wa kina kuhusu mahitaji halisi ya walimu. Msisitizo huu unaonyesha uelewa mzuri wa kuwa mabadiliko endelevu ya sekta ya elimu yanahitaji msingi imara wa taarifa sahihi na za kuaminika.

Utafiti wa kina unaojumuisha idadi, aina na viwango vya walimu unaongeza uwezo wa TSC kutoa ushauri wa kitaalamu unaoweza kusaidia serikali kupanga na kutekeleza hatua madhubuti za kuboresha elimu.

Tafiti ni zana muhimu sana katika kuandaa mipango ya masuala ya walimu, kubaini changamoto zinazohitaji kushughulikiwa,

na kuhakikisha rasilimali zinatumiwa kwa ufanisi. Bila matokeo ya utafiti makini, maamuzi yanaweza kuwa ya dharura au yasiyo na mwendo wa muda mrefu, jambo linaloweza kudhoofisha juhudi za kitaifa za kuboresha elimu. Utafiti mzuri hutoa takwimu thabiti na mwongozo unaohitajika kuimarisha sera na utekelezaji wa mpango wa elimu.

Kwa hiyo, witowetuni kwa TSC kuhakikisha inatekeleza jukumu hili ipasavyo, kwa weledi na kwa kuzingatia usahihi wa taarifa zinazokusanywa. Utekelezaji wa jukumu hili kwa ufanisi utaiwezesha serikali kupata ushauri sahihi na wa kuaminika unaoweza kuongoza hatua za kuboresha elimu nchini, kuhakikisha kila hatua inayochukuliwa inatokana na data halisi na mahitaji ya kweli ya sekta.

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya
Edwin Mgendera

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

Na Mwandishi Wetu – Dodoma

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mhe. Reuben Kwagilwa, amelelekeza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kuhakikisha kuwa kunakuwepo na uwiano sahihi wa usambazaji wa walimu katika Serikali za Mitaa na shule zote nchini, ili kila mtoto apate elimu bora bila kujali eneo analoishi.

Akizungumza tarehe 25 Novemba 2025 wakati alipokutana na Wajumbe wa Tume, Menejimenti na Watumishi wa Tume hiyo, Mhe. Kwagilwa alisema hatua hiyo ni muhimu katika kuondoa tofauti zilizopo kati ya shule zenye walimu wengi na zile zenye walimu wachache.

“Katika kutekeleza jukumu lenu la kusimamia na kuendeleza utumishi wa walimu, hakikisheni kunakuwepo kwa uwiano mzuri katika shule zetu. Tusiendeleze kuwa na shule za mijini zikiwa na walimu wengi huku shule za vijijini zikiwa na upungufu mkubwa,” alisisitiza.

Ameongeza kuwa wakati wa kampeni, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliahidi kuajiri walimu 7,000 ndani ya siku 100 ili kuboresha elimu, ikiwemo

NAIBU WAZIRI KWAGILWA AAGIZA TSC KUHAHAKIKISHA UWIANO SAWA WA WALIMU NCHINI



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Reuben Kwagilwa (kushoto) akisalimiana na Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama katika ziara yake ya kukutana wa Wajumbe na watumishi wa Tume tarehe 25 Novemba 2025.

kutekeleza mkakati wa kuhakikisha kila mwanafunzi wa darasa la tatu anaweza kusoma, kuandika na kuhesabu bila changamoto.

Aidha, Naibu Waziri ameitaka

Tume kufanya utafiti na tathmini ya kina kuhusu mahitaji halisi ya watumishi wa sekta ya elimu, ili kuishauri Mamlaka ya Ajira juu ya idadi, aina na ngazi za walimu wanaohitajika katika maeneo mbalimbali.

Katika hatua nyingine, Mhe. Kwagilwa ameiagiza Tume kuhakikisha kuwa mashauri yote ya kinidhamu na kiutumishi yanamalizika katika ngazi ya Tume, kwa kuzingatia misingi ya haki, uwazi na uadilifu.

Awali, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume, alisema TSC inasimamia jumla ya walimu 289,984, wakiwemo walimu 186,207 wa shule za msingi na walimu 103,777 wa shule za sekondari.

Aidha, kuhusu kupandisha vyeo, Mwl. Nkwama alisema kuwa kwa mwaka 2024/2025, jumla ya walimu 97,992 walipandishwa vyeo— kati yao 61,679 ni wa shule za msingi na 36,313 ni wa sekondari. Aliongeza kuwa mwaka 2023/2024, walimu 158,916 walipandishwa vyeo, huku mwaka 2022/2023 walimu 65,925 wakipandishwa vyeo.



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Reuben Kwagilwa (kulia) akipokea ua kama ukaribisho kutoka kwa mtumishi wa TSC, Enid Geofrey wakati wa ziara yake ya kukutana wa Wajumbe na watumishi wa Tume tarehe 25 Novemba 2025.

NAIBU WAZIRI KWAGILWA AAGIZA TSC KUHAJIKISHA UWIANO SAWA WA WALIMU NCHINI



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Reuben Kwagilwa (katikati) akiwa katika mazungumzo na Mwenyekiti wa TSC, Prof. Masoud Hadi Muruke (kushoto) na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama wakati wa ziara yake ya kukutana na Wajumbe na watumishi wa Tume tarehe 25 Novemba 2025.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu akitoa neno la kumkaribisha Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Mhe. Reuben Kwagilwa, katika kikao kilichofanyika tarehe 25 Novemba 2025, jijini Dodoma.



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Reuben Kwagilwa akizungumza na Wajumbe na Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 25 Novemba 2025, jijini Dodoma.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika kikao kilichofanyika tarehe 25 Novemba 2025, jijini Dodoma.

NAIBU WAZIRI KWAGILWA AAGIZA TSC KUHAJIKISHA UWIANO SAWA WA WALIMU NCHINI



Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (mstari wa mbele) wakiwa katika kikao cha Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Mhe. Reuben Kwagilwa tarehe 25 Novemba 2025.



Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu wakiwa kwenye kikao na Naibu Waziri tarehe 25 Novemba 2025, jijini Dodoma.

NAIBU WAZIRI KWAGILWA AAGIZA TSC KUHAJIKISHA UWIANO SAWA WA WALIMU NCHINI



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Mhe. Reuben Kwagikwa (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu mara baada ya kikao kilichofanyika tarehe 25 Novemba 2025, jijini Dodoma.



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Mhe. Reuben Kwagikwa (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 25 Novemba 2025, jijini Dodoma.

NAIBU WAZIRI KWAGILWA AAGIZA TSC KUHAJIKISHA UWIANO SAWA WA WALIMU NCHINI



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Mhe. Reuben Kwavilwa (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 25 Novemba 2025, jijini Dodoma.

MAGEUZI YA SERIKALI KWENYE ELIMU YALETA MWANGAZA MPYA SHULENI, WALIMU WASEMA “TUNAONA TOFAUTI”

Na mwandishi wetu – Kilimanjaro.

Katika Mkoa wa Kilimanjaro, sauti za walimu zinaanza kutoa taswira mpya kuhusu mabadiliko yanayoendelea katika sekta ya elimu. Hatua zilizochukuliwa na serikali katika kuboresha huduma, mazingira ya kazi na mifumo ya usimamizi zimeanza kuonekana wazi katika maisha ya walimu na uendeshaji wa shule.

Kupitia mahojiano maalum na wakuu wa shule, Mwalimu Abdallah Seif Momboka wa Shule ya Sekondari Kifaru (Mwanga), Mwalimu Justice Kikani wa Sekondari Kilamfua (Rombo), na Mwalimu Magdalena Mushi wa Shule ya Msingi Huruma (Rombo)—inaonekana kuwa mabadiliko haya yameleta mwamko mpya katika utendaji wa walimu na uongozi wa shule.

Mwalimu Momboka, akiwa na uzoefu wamudamrefu katika uongozi wa shule, anaanza kwa kueleza jinsi mazingira ya kazi yalivyobadilika katika miaka ya karibuni. Anasema kuwa Shule ya Kifaru sasa ina miundombinu iliyoboreshwa kwa kiwango kinachoridhisha. Madarasa yameongezeka, maabara zimekamiliwa, na vifaa vya kufundishia vimepatikana kwa wingi



Mwalimu Abdallah Seif Momboka akizungumza kuhusu maboresho ya mazingira ya kazi na morali ya walimu katika Shule ya Sekondari Kifaru, Mwanga.

zaidi.

Lakini zaidi ya yote, anasisitiza kuwa maboresho ya kiutumishi ambayo kwa miaka mingi yalikuwa kilio cha walimu sasa yameanza

kushughulikiwa kwa kasi zaidi na serikali. Kupandishwa kwa madaraja kwa wakati, kurekebisha kwa mishahara, kushughulikiwa kwa malimbikizo, na utoaji wa stahiki mbalimbali kwa uharaka vimeongeza morali ya walimu kwa kiwango kikubwa. “Hata mimi nimepandishwa madaraja kwa mserekeo. Ni jambo ambalo hapo zamani lilikuwa kama bahati nasibu, lakini sasa limekuwa utaratibu unaoeleweka. Limetupa moyo wa kufanya kazi kwa bidii,” anasema kwa msisitizo.

Katika Wilaya ya Rombo, Mwalimu Justice Kikani naye anakiri kwamba kasi ya maboresho imekuwa ya kutia matumaini. Anaeleza kuwa kwa miaka mingi walimu walikuwa wakitumia muda mwingi na nguvu nyingi kufuatilia stahiki zao, hasa fedha za likizo. Mara nyingi walimu walienda likizo na kurudi kazini bila kupokea malipo yao kwa wakati. Hali hiyo sasa imebadilika.



Mwalimu Justice Kikani wa Sekondari Kilamfua, Rombo, akiainisha namna malipo ya stahiki mbalimbali yanavyotolewa kwa wakati na jinsi hali hiyo ilivyowapa walimu matumaini mapya.

INAENDELEA UK. 9

MAGEUZI YA SERIKALI KWENYE ELIMU YALETA MWANGAZA MPYA SHULENI, WALIMU WASEMA “TUNAONA TOFAUTI”

INATOKA UK. 8

“Leo hii unakuta malipo ya likizo yanatoka miezi miwili kabla hata ya tarehe ya kuanza likizo. Hili ni jambo kubwa,” anafafanua. Anabainisha kuwa ingawa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) inasimamia masuala ya kiutumishi, ni serikali kupitia mifumo yake ya malipo inayowajibika kutoa fedha hizo, jambo linaloonyesha dhamira ya kuboresha ustawi wa mwalimu.

Mwalimu Magdalena Mushi naye anaeleza jinsi mfumo wa kidijitali wa TSCMIS ulivyoleta nafuu kubwa kwa walimu. Kupitia mfumo huu, mwalimu anaweza kutuma maombi ya madaraja, kufuatilia taarifa zake za kiutumishi, au kuwasilisha changamoto mbalimbali bila kulazimika kwenda ofisini.

Anasema kuwa hali hii imepunguza mlolongo wa urasimu uliokuwa ukisababisha kuchelewesha maamuzi. “Huu ni mfumo ambao umetuheshimu sisi walimu. Unatuondolea gharama na muda tuliokuwa tunapoteza,” anasema.

Kwa upande wa ushirikiano na TSC wilaya, viongozi hawa wote wanakiri kuwa uimara wa mawasiliano na urahisi wa kupokea maelekezo umezidisha ufanisi katika utendaji. Mwalimu Momboka anatoa mfano wa taarifa za TANGE zinazoratibiwa kwanza katika ngazi ya shule kabla ya kupelekwa TSC, akieleza kuwa majukumu ya usimamizi wa nidhamu, kupandishwa madaraja, kubadili cheo au kazi, na vibali vya kustaafu yamekuwa yakitekelezwa kwa ukaribu na weledi mkubwa.

Hata hivyo, pamoja na hatua hizi chanya, changamoto za kimienendo miongoni mwa walimu, hasa wale vijana, bado zipo. Mwalimu Momboka anakiri kuwa vijana wengi wanahitaji mwongozo wa karibu ili kuelewa misingi ya taaluma ya ualimu.

Anaeleza kuwa njia wanazotumia kuwasaidia walimu kuzingatia maadili ya kazi ni rafiki na zinafanya kazi vizuri. “Tunawalea, tunawaelekeza, hatutumii nguvu.

Mara nyingi tukitoa elimu tu mambo yanakwisha,” anasema. Mwalimu Kikani anaongeza kwa kutoa mfano wa walimu wanaovaa mavazi yasiyoendana na maadili ya kazi yao, wakidhani ni jambo la kawaida. Anasema kuwa maelekezo ya kiungwana huwafanya kubadilika haraka.

Mwisho wa mazungumzo haya unaibua mtazamo wa pamoja kuhusu mustakabali wa elimu nchini. Walimu hawa wanakubali kuwa serikali imepiga hatua, lakini bado ipo nafasi kubwa ya kuboresha zaidi. Mwalimu Momboka anashauri serikali kuongeza rasilimali watu na fedha kwa TSC ili iweze kutekeleza majukumu yake bila kuchelewa, huku Mwalimu Magdalena akisisitiza

umuhimu wa kuongeza vifaa vya TEHAMA katika shule, akitaja projector, kompyuta na mashine za kupiga nakala kama nyenzo muhimu za kuboresha ufundishaji na utawala.

Kwa ujumla, kauli za viongozi hawa zinajenga picha ya tasnia ya elimu inavyopiga hatua kutoka changamoto za muda mrefu na kuingia katika hatua mpya yenye matumaini zaidi. Mwalimu anaonekana kuanza kuheshimiwa, kusikilizwana kutekelezewa hakizake kwa wakati. Ingawa safari haijafika mwisho, hatua zinazoendelea kuchukuliwa na serikali zinaashiria mwelekeo sahihi kuelekea kwenye mfumo wa elimu utakaoweza kilicho bora katika kizazi kijacho.



Mwalimu Magdalena Mushi wa Shule ya Msingi Huruma akielezea faida za mfumo wa kidijitali wa TSCMIS katika kupunguza urasimu na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kiutumishi kwa walimu.

KATIBU WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU ATOA WITO WA USHIRIKIANO NA UWAJIBIKAJI KWA WATUMISHI

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, amewataka watumishi wa Tume hiyo kote nchini kuendelea kushirikiana, kuwa waadilifu na kuwajibika katika utekelezaji wa majukumu yao ili kuongeza ufanisi wa taasisi hiyo muhimu katika sekta ya elimu.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Kwanza wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume kwa mwaka 2025/2026, uliofanyika katika Ukumbi wa Mabeyo, Dodoma, Mwl. Nkwama alisema baraza hilo ni jukwaa muhimu kwa watumishi kujadili changamoto, kutoa mawazo na kubuni mikakati ya kuboresha utendaji kazi wa Tume.

“Tuitumie fursa ya mkutano huu kujadili kwa uwazi, tukilenga kuleta suluhisho endelevu kwa changamoto tunazokutana nazo katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku,” alisema Mwl. Nkwama.

Katibu huyo alitoa pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, na Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa uongozi wao makini unaoendelea kuimarisha sekta ya elimu na kuwezesha taasisi kama TSC kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

“Tuna imani kuwa chini ya uongozi



Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama, akitoa hotuba ya ufunguzi wa Mkutano wa Kwanza wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume kwa mwaka 2025/2026, uliofanyika tarehe 13 Novemba 2025 katika Ukumbi wa Mabeyo, jijini Dodoma.

wa Serikali ya Awamu ya Sita, sekta ya elimu na hususan Tume ya Utumishi wa Walimu itaendelea kupata nguvu mpya na rasilimali muhimu katika kutekeleza majukumu yake,” alisema.

Aidha, Mwl. Nkwama aliwapongeza watumishi wote wa Tume kwa kujituma licha ya changamoto za kiutendaji, akisema juhudi zao zimeiwezesha Tume kuendelea kutoa huduma bora kwa walimu nchini.

“Pamoja na changamoto, mmeendelea kujitoa na kuhakikisha kazi za Tume zinaendelea kutekelezwa kwa ufanisi. Hongereni sana kwa moyo huo wa uzalendo na uadilifu,” alisema Mwl. Nkwama huku akishangiliwa na wajumbe wa baraza.

Miongoni mwa ajenda zilizojadiliwa katika mkutano huo ni pamoja na kupitia na kuthibitisha taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/25, rasimu ya Mpango Mkakati wa Tume kwa 2026/27–2030/31, na taarifa za utawala na rasilimali watu.



Katibu wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Bw. Nuhu Mlekwa, akitoa neno la utangulizi wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi, uliofanyika tarehe 13 Novemba 2025 katika Ukumbi wa Mabeyo, jijini Dodoma.

KATIBU WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU ATOA WITO
WA USHIRIKIANO NA UWAJIBIKAJI KWA WATUMISHI

Mwakilishi wa Baraza Kuu la Wafanyakazi Serikalini, Bw. Brendan Maro, akitoa salamu za Baraza Kuu wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu, tarehe 13 Novemba 2025, katika Ukumbi wa Mabeyo, jijini Dodoma.



Washiriki wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu wakiimba kwa pamoja wimbo wa mshikamano wa wafanyakazi wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi, uliofanyika tarehe 13 Novemba 2025 katika Ukumbi wa Mabeyo, jijini Dodoma.



Washiriki wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu wakiwa wamesimama kwa utulivu kama ishara ya kumuombea na kumkumbuka aliyekuwa Mtumishi wa Tume na Mjumbe wa Baraza, aliyefariki dunia miezi michache iliyopita, wakati wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi uliofanyika tarehe 13 Novemba 2025 katika Ukumbi wa Mabeyo, jijini Dodoma.

KATIBU WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU ATOA WITO WA USHIRIKIANO NA UWAJIBIKAJI KWA WATUMISHI



Washiriki wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu wakifuatilia kwa makini mijadala mbalimbali wakati wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi, uliofanyika tarehe 13 Novemba 2025 katika Ukumbi wa Mabeyo, jijini Dodoma.



Mwenyekiti wa TUGHE Tarvi la Tume ya Utumishi wa Walimu, Bw. Francis Gwankisa, akitoa mchango wake katika mijadala wakati wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume, uliofanyika tarehe 13 Novemba 2025 katika Ukumbi wa Mabeyo, jijini Dodoma.

Afisa Mchumi Mkuu kutoka Kitengo cha Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Bw. Elia Malaki, akiwasilisha mada wakati wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume, uliofanyika tarehe 13 Novemba 2025 katika Ukumbi wa Mabeyo, jijini Dodoma.

KATIBU WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU ATOA WITO WA USHIRIKIANO NA UWAJIBIKAJI KWA WATUMISHI



Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa Baraza la Wafanyakazi baada ya ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume, tarehe 13 Novemba 2025 katika Ukumbi wa Mabeyo, jijini Dodoma.

KIKAO CHA PILI CHA KAMATI YA UTAWALA NA FEDHA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU CHAFANYIKA DODOMA



Mwenyekiti wa Kikao cha Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma, Bi. Mariam Mwanilwa, akiongoza kikao kilichofanyika tarehe 14 Novemba 2025 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imefanya kikao chake cha pili kwa mwaka wa fedha 2025/2026 tarehe 14 Novemba 2025.

Kikao hicho kilichofanyikia katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma, kiliongozwa na, Bi. Mariam Mwanilwa, na kuhudhuriwa na Makamishna wa Tume, Bi. Bahati Mgongolwa na Bw. Aggrey Mleli pamoja na Menejimenti ya Tume.

Katika kikao hicho, wajumbe walijadili ajenda kadhaa muhimu ikiwemo taarifa ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu kwa robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2025/2026, Mpango wa Mafunzo wa Tume kwa mwaka 2025/26 hadi 2029/30, taarifa ya utekelezaji wa Mpango na bajeti ya Tume kwa kipindi cha robo ya kwanza, pamoja na kupitia rasimu ya Mpango Mkakati wa Tume kwa mwaka 2026/2027 hadi 2030/2031.

Masuala hayo yote yamelenga kuimarisha utendaji wa Tume katika maeneo ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ili kuboresha huduma kwa walimu nchi nzima.

Kikao hicho kilielezwa kuwa ni hatua muhimu katika maandalizi ya Mkutano wa Tume iliofanyika tarehe 24 hadi 28 Naovemba, 2025, ambapo taarifa na mapendekezo yaliyowasilishwa yalipitiwa kwa kina kabla ya kupitishwa rasmi.



Katibu wa Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ambaye pia ni Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama, akizungumza wakati wa kikao cha kamati hiyo kilichofanyika tarehe 14 Novemba 2025 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

KIKAO CHA PILI CHA KAMATI YA UTAWALA NA FEDHA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU CHAFANYIKA DODOMA



Washiriki wa Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma wakiwa kwenye kikao cha kamati hiyo kilichofanyika tarehe 14 Novemba 2025 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

NAIBU WAZIRI KWAGILWA ATEMBELEA MRADI WA UJENZI WA JENGO LA TSC, AAGIZA SUMA JKT KUKAMILISHA KWA WAKATI

Na Mwandishi Wetu – Dodoma

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Reuben Kwagilwa tarehe 25 Novemba, 2025 ametembelea mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Makao Makuu unaojengwa katika eneo la Njedengwa jijini Dodoma na kutoa agizo kwa mkandarasi SUMA JKT kuhakikisha anakamilisha mradi huo ndani ya muda wa nyongeza waliuomba.

Akizungumza mara baada ya kukagua mradi huo, Mhe. Kwagilwa alisema kuwa mkandarasi anatakiwa kutumia vyema muda wa nyongeza wa miezi sita aliuomba pamoja na marekebisho mengine ya mkataba yanayolenga kuongeza kasi ya ukamilishaji wa ujenzi huo na kuongeza kuwa Serikali inatarajia ujenzi huo kukamilika kama ilivyopangwa bila kusababisha ucheleweshaji mwingine.

Aidha, alielekeza Tume ya Utumishi wa Walimu kufanya vikao na mkandarasi kila mwezi ili kujadili changamoto na kufuatilia maendeleo ya mradi.

Akitoa taarifa ya ujenzi kwa niaba ya SUMA JKT, mwakilishi wa mkandarasi alisema kuwa mradi umefikia asilimia 70. Alifafanua kuwa kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa msingi, kusimamisha kuta kutoka ngazi ya chini hadi hatua ya kuezeka, ufungaji wa paa, ujenzi wa kuta (block works), upigaji lipu zaidi ya asilimia 50, pamoja na ufungaji wa fremu na grill za madirisha.

Awali, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa mradi huo una thamani ya shilingi bilioni 6.4 na ulipaswa kukamilika ndani ya miezi 18. Alisema kuwa hadi tarehe 25 Novemba, 2025 kiasi cha shilingi bilioni 2.8 kimelipwa sawa na asilimia 44.27 ya thamani ya mkataba.

Mwl. Paulina alisema kuwa mkandarasi amewasilisha ombi la kufanya marekebisho ya mkataba



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Mhe. Reuben Kwagilwa (mwenye fimbo mkononi) akiwa katika ukaguzi wa ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 25 Novemba 2025, jijini Dodoma.

pamoja na kuongezewa muda ameongezewa muda hadi tarehe 1 wa kukamilisha mradi ambapo Juni 2026.

NAIBU WAZIRI KWAGILWA ATEMBELEA MRADI WA UJENZI WA JENGO LA TSC, AAGIZA SUMA JKT KUKAMILISHA KWA WAKATI



Naibu Waziri Mhe. Reuben Kwagilwa akitoa maelekezo kwa Tume ya Utumishi wa Walimu na Mkandarasi SUMA JKT wakati wa ziara yake ya ukaguzi wa maendeleo ya mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Tume Makao Makuu tarehe 25 Novemba 2025, jijini Dodoma.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke akitoa maelezo wakati wa kikao cha Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Mhe. Reuben Kwagilwa, TSC na Mkandarasi wa ujezi wa jengo la Ofisi ya Tume Makao Makuu, SUMA JKT wakati wa ziara ya Naibu Waziri kwenye mradi tarehe 25 Novemba, 2025.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akitoa ufafanuzi juu ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi kwa Naibu Waziri wakati wa ziara iliyofanyika tarehe 25 Novemba 2025, jijini Dodoma.



Wajumbe na Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu wakiwa katika kikao wakati wa ziara ya Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Mhe. Reuben Kwagilwa, kwenye mradi wa ujenzi wa ofisi za TSC Makao Makuu jijini Dodoma tarehe 25 Novemba 2025.



NAIBU WAZIRI KWAGILWA ATEMBELEA MRADI WA UJENZI WA JENGO LA TSC, AAGIZA SUMA JKT KUKAMILISHA KWA WAKATI



Naibu Waziri Mhe. Reuben Kwagikwa (mwenye fimbo mkononi) akipitia ramani ya jengo la Ofisi za TSC Makao Makuu wakati wa ziara yake katika mradi wa ujenzi wa jengo la Tume tarehe 25 Novemba 2025, jijini Dodoma.

Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu na Watumishi wa Tume wakiwa katika ziara ya Naibu Waziri Mhe. Reuben Kwagikwa kwenye ujenzi wa Ofisi za Tume Makao Makuu tarehe 25 Novemba 2025.



Hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa jengo la ofisi za TSC Makao Makuu kufikia tarehe 25 Novemba, 2025.

TSC YAJIDHINISHA RASIMU YA MPANGO MKAKATI MPYA WA MIAKA MITANO



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke (Katibu) akiongoza kikao cha Tume kilichofanyika Dodoma hivi karibuni. Pichani, wa kwanza kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa Tume, Bi. Bahati Mgongolwa na upande wa kulia ni Katibu wa Tume. Mwl. Paulina Nkwama.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akitoa taarifa ya shughuli zilizofanyika katika Mkutano wa Tume uliofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.

Na Mwandishi wetu, Dodoma.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeboresha na kuidhinisha rasimu ya Mpango Mkakati mpya utakaoiongoza Tume hiyo kwakipindi chamiaka mitano kuanzia mwaka 2026/27 hadi 2030/31, ikiwa ni hatua muhimu katika kupanga mwelekeo wa utendaji wa Tume na kuboresha usimamizi wa rasilimali watu katika sekta ya elimu.

Akizungumza baada ya Wajumbe wa Tume kupitia na kujadili rasimu hiyo, Mwenyekiti wa Tume, Prof. Masoud Muruke, aliipongeza Menejimenti kwa kazi kubwa ya maandalizi huku akisisitiza umuhimu wa kuzingatia maoni ya wadau pamoja na marekebisho yaliyotolewa

na Wajumbe.

"Nawapongeza kwa kazi nzuri ya maandalizi ya Mpango Mkakati wa Tume hadi kufikia leo hii, haikuwa kazi nyepesi... Nyaraka hii ni muhimu katika maandalizi ya Mpango na Bajeti katika kipindi cha miaka mitano ijayo," alisema Prof. Muruke. Pia alisisitiza kuingizwa kwa masuala ya maendeleo ya sayansi na teknolojia katika utekelezaji wa Mpango huo ili kuongeza ufanisi wa Tume katika kutoa huduma.

Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama, aliwashukuru Wajumbe kwa kuupitia kwa umakini na kuuidhinisha baada ya kutoa maoni mbalimbali yatakayoboresha Mpango huo mpya. Alieleza kuwa rasimu hiyo imeandaliwa baada ya kukamilika kwa Mpango Mkakati

uliotangulia.

Katika hatua nyingine, Prof. Muruke aliipongeza Sekretarieti ya Tume kwa maandalizi mazuri ya mkutano huo ambao pamoja na mambo mengine ulipitia na kuamua rufaa 22 za walimu.

Awali, Mwl. Nkwana alifafanua kuwa katika kipindi cha siku tano, Wajumbe walijadili jumla ya rufaa 22 ambapo rufaa 10 zilipitishwa, 5 zikakataliwa, 4 zikaonekana zimekatwa nje ya muda, huku 3 zikirejeshwa kwa ajili ya kuanza upya kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu.

Hatua hiyo inaendelea kuthibitisha dhamira ya TSC kuboresha mifumo yake ya utendaji, kuongeza uwazi na kuhakikisha haki inatolewa kwa walimu nchini.



Washiriki wa Mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu uliofanyika hivi karibuni jijini Dodoma wakiwa kwenye kikao hicho.



Mtaalamu kutoka Chuo cha Mipango Maendeleo vijijini wakitoa wasilisho la mada kuhusu rasimu ya Mpango Mkakati wa Tume hivi karibuni jijini Dodoma hivi karibuni.

SERIKALI YA AWAMU YA SITA YATATUA CHANGAMOTO ZA WALIMU WA UYUI



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Uyui, Bw. Henry Wamara, akifanya mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka Makao Makuu ya Tume, hivi karibuni.

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume, Bw. Henry Wamara, akiwa katika picha ya pamoja na Maafisa wa TSC ngazi ya Wilaya ya Uyui baada ya mahojiano. Kushoto ni Kalunde Shabani Kanyaga na kulia ni Magreth Jarome Katanga.

Na Mwandishi Wetu, Uyui

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kutekeleza kwa ufanisi mpango wa kutatua changamoto za muda mrefu zilizokuwa zikiwakabili walimu, hususan katika upandishwaji wa madaraja.

Hayo yamebainika hivi karibuni katika mahojiano maalum kati ya walimu wa Wilaya ya Uyui, Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wilayani humo, pamoja na

Maafisa Habari kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha Tume hiyo.

Mwalimu Leonard Songe Affa wa Shule ya Msingi Goweke alisema kwa muda mrefu alikuwa akikumbana na ucheleweshwaji wa madaraja, lakini Serikali ya Awamu ya Sita imemaliza tatizo hilo kwa kumpandisha madaraja kwa mfululizo hadi kufikia kiwango alichostahili.

"Naishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kunitatulia changamoto ya kutopandishwa daraja kwa muda mrefu. Hali hii imenipa ari kubwa ya

kufanya kazi kwa bidii," alisema.

Naye Mwalimu Wema Jaliko wa Shule ya Msingi Ulimakafu alisema kuwa hatua ya kupandishwa madaraja kwa utaratibu wa mserekeo imewajengea walimu wengi matumaini na kuongeza moyo wa kufanya kazi kwa weledi.

"Tumepewa mserekeo wa madaraja yetu. Sasa moyo wa kufanya kazi umeongezeka na tunafurahia kazi yetu kwa sababu haki zilizokuwa zimecheleweshwa sasa tumepatiwa," alifafanua.

Kwa upande wake, Mwalimu Mbaraka Said Semroki wa Shule ya Msingi Mbiti aliishukuru Serikali kwa kumwezesha kupandishwa madaraja aliyokuwa ameyakosa kwa miaka mingi.

"Nimepandishwa mpaka daraja la mwisho la kada yangu. Nina morali ya kazi na ninaendelea kufanya kazi kwa furaha na amani baada ya changamoto yangu kutatuliwa," alisema kwa msisitizo.

Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Uyui, Bw. Henry Wamara, alithibitisha hatua kubwa iliyopigwa na Serikali katika kushughulikia madaraja ya walimu.

Amesema kuwa kuanzia mwaka 2021 hadi 2025, jumla ya walimu 2,168 wamepandishwa madaraja wilayani Uyui, wakiwemo walimu 1,635 wa shule za msingi na 533 wa shule za sekondari.



Mwalimu Mbaraka Said Semroki wa Shule ya Msingi Mbiti, mmoja wa walimu waliofaidika na upandishaji wa madaraja.



Mwalimu Leonard Songe Affa wa Shule ya Msingi Goweke, akieleza namna Serikali ilivyotatua changamoto yake ya upandishaji madaraja.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz **Tovuti:** www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu